



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

UCHAGUZI MDOGO WA UBUNGE MAJIMBO MAWILI (2) KWENYE HALMASHAURI MBILI (2) MKOANI KIGOMA NA UDIWANI KATIKA KATA TANO (5) ZA HALMASHAURI TANO (5) ZILIZOKO KATIKA MIKOA MINNE (4) TAREHE 16 MEI, 2021

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa Majimbo mawili (2) ya Muhambwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo na Buhigwe katika Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe Mkoani Kigoma kuwa itafanya Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Majimbo hayo pamoja na Uchaguzi Mdogo wa Udiwani katika Kata tano (5) za Buziku, Halmashauri ya Chato na Bugalama katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita Mkoani Geita, Igunga katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga Mkoani Tabora, Miuta katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, Mkoani Mtwara na Ligoma katika Halmashauri ya Tunduru, Mkoani Ruvuma siku ya Jumapili, tarehe **16/05/2021**. Upigaji Kura utafanyika katika vituo vilivyotumika katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Vituo vitafunguliwa saa 1:00 Asubuhi na kufungwa saa 10:00 jioni.

Mambo ya kuzingatia wakati wa Uchaguzi.

1. Watakaoruhusiwa kupiga kura ni wale walioandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga kura na wana kadi za Kupigia Kura.
2. Aidha, waliopoteza kadi zao za kupigia kura au kuharibika, wanaruhusiwa kutumia vitambulisho mbadala ambavyo ni hati ya kusafiria, Leseni ya Udereva au Kitambulisho cha Taifa ambacho majina yote matatu yanafanana na yaliyomo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura
3. Mpiga Kura anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni.
4. Baada ya kumaliza kupiga kura, Mpiga Kura anatakiwa kuondoka eneo la Kituo cha Kupigia Kura
5. Mpiga Kura anatakiwa afuate maelekezo yote atakayopewa na Msimamizi wa Kituo.
6. Wenye ulemavu, Wazee, Wagonjwa, Wajawazito na Akina mama wanaonyonyesha ambao watakuwa na watoto kituoni watapewa kipaumbele.

Dkt. Wilson Mahera Charles

MKURUGENZI WA UCHAGUZI